

## BASIL

*Ocimum basil Linn.*



### Utangulizi

Basil ni mmea ambao una harufu kali ambao hulimwa zaidi katika nchi za Egypt na marekani.. Mmea huu hulimwa kwa ajili ya harufu yake na ladha ya kipekee. Nchini Tanzania, mmea huu haujaanza kulimwa bali

hupatikana porini na kujulikana kama *vumbasa* au *mfumbasi*

### Umbile la mmea

Mmea wa basil hukua na kufika urefu wa sentimita 60. Una matawi madogo madogo na kuufanya uonekane kama kichaka kidogo. Mmea wa basil huweza kuwa na rangi tofauti za majani kutegemeana na aina. Huweza kuwa katika rangi ya kijani iliyokolea au zambarau.

### Uzalishaji

Basil huoteshwakwa mbegu na hustawi vizuri katika udongo wenyre rutuba. Mbegu zipandwe katika mistari ilio umbali wa sentimita 90. Nafasi kati ya mmea hadi mmea ni umbali wa sementimita 30. Mbegu huota baada ya siku 5 hadi 7 tangu kupandwa.

Mmea wa basil hutoa maua mapema, hivyo maua yatolewe ili kuepuka kutoa mbegu mapema. Pia mmea ukatwe hadi urefu wa sintimita 15 hadi 20 ili kuupa nguvu ya kukua vizuri. Mmea huwa tayari kuchumwa miezi 2 baada ya kupandikizwa. Uvunaji hufanywa kwa kuchuma majani machanga kila inapohitajika. Mmea ukishakua vizuri matawi huweza kuvunwa kwa kukatwa na kuning'niwa katika kivuli, chumba chenye hewa safi au kutandazwa

kwenye chekeche. Baada ya kukauka matawi hupukutuliwa ili kupata majani na maua makavu. Majani hayo yahifadhiwe katika chombo kinachofunga vizuri.

### Matumizi

Mmea wa Basil una mafuta na kemikali za aina mbalimbali Kemikali hizo hutoa harufu na ladha ambazo huufanya mmea huu kutumika katika majumbani na viwandani.

Majani mabichi na makavu ya Basili hutumika katika vyakula na matibabu mbalimbali. Katika vyakula, hutumika zaidi katika vyakula vinavyopikwa kwa nyanya, salad ya matango, mayai, jibini n.k

Mafuta yanayopatikana katika mmea wa basil hutumika katika bidhaa za viwandani kama manukato,sabuni, na vipodozi, pia ni dawa nzuri ya kufukuza wadudu kama mbu. Basil pia hutumika katika kupunguza maumivu, kutapika, uchovu wa akili na maumivu ya kichwa.

**Kwa maelezo zaidi wasilia na:**  
**Wizara ya Kilimo, Chakula, na Ushirika**  
**Idara ya Uendelezaji Mazao**  
**P.O.BOX 9192**  
**Dar Es Salaam.**  
**E mail: cps@kilimo.go.tz**